



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA

NA LESENI (BRELA)

# TANGAZO

Wakala ya Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) inapenda kuarifu umma kuwa imekamilisha mfumo wa usajili wa Makampuni hivyo huduma zote za usajili na za baada ya usajili zitatolewa kwa njia ya Mtandao. Mfumo utamwezesha Mteja kupata huduma popote alipo. BRELA itaanza kutoa huduma za usajili wa makampuni na za baada ya usajili rasmi kwa njia ya Mtandao kuanzia tarehe 1 Februari, 2018.

Ili kuweza kutumia mfumo huu ni lazima watumiaji wazingatie yafuatayo:-

- (i) Kuwa na Namba ya Utambulisho wa Utaifa (National Identification Number (NIN) inayotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
- (ii) Ikiwa unatarajia kuwa Mkurugenzi wa Kampuni (Director) uwe tayari una Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN) inayotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).
- (iii) Wakati unaandaa Malengo na Katiba ya Kampuni (Memorandum and Article of Association) hakikisha malengo unayojiwekea yameendana na shughuli unazozichagua kwenye mfumo wa ORS kwa mujibu wa 'ISIC classification' ambayo itapatikana kwenye mtandao na kwenye Tovuti ya BRELA

Kwa maelezo zaidi tafadhali tembelea tovuti ya BRELA; [www.brela.go.tz](http://www.brela.go.tz).

**Imetolewa na:**

**AFISA MTENDAJI MKUU**

**Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)**

**S.L.P. 9393**

**Dar es Salaam.**

**Simu: +255-22-2181344, 2180113, 2180141, 2180048,**

**Nukushi: +255-22-2180371**

**Barua Pepe: [usajili@brela.go.tz](mailto:usajili@brela.go.tz); [ceo@brela.go.tz](mailto:ceo@brela.go.tz)**

**Tovuti: [www.brela.go.tz](http://www.brela.go.tz)**